**HOTUBA YA UFUNGUZI WA MKUTANO WA NNE WA BARAZA LA WAFANYAKAZI WA MAMLAKA YA BIMA (TIRA) ILIYOTOLEWA NA MWENYEKITI WA BODI YA TAIFA YA BIMA DR. YAMUNGU KAYANDABILA, FEBRUARI 10, 2017 KATIKA UKUMBI WA KIMATAIFA WA MWALIMU JULIUS NYERERE, DAR ES SALAAM.**

**Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi - TIRA,**
**Makamu Mwenyekiti wa Baraza,**
**Wajumbe wa Baraza,**
**Wajumbe kutoka TUGHE,**
**Mjumbe kutoka Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA),**
**Mabibi na Mabwana,**
**Habari za Asubuhi;**

Awali ya yote, napenda kuwashukuru kwa kunialika ili nifungue mkutano huu.

Nachukua nafasi hii kuwapongeza kwa kuwa na Baraza la Wafanyakazi TIRA. Kipekee nawashukuru Wajumbe kutoka TUGHE Mkoa wa Dar es Salaam pamoja na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) kwa kufanya kazi kwa karibu na Tawi la TUGHE la TIRA ili kuhakikisha Baraza letu la Wafanyakazi linafanya kazi kama inavyotakiwa.

**Ndugu wajumbe**, Baraza hili ni jukwaa muhimu sana mahala pa kazi kwani ni kiunganishi kati ya Menejimenti na Wafanyakazi. Ni matumaini yangu kuwa mtaendelea kushirikiana ili kuleta ufanisi kwa Mamlaka na Taifa kwa ujumla. Hata hivyo ikumbukwe kuwa Serikali inazingatia sana suala la taasisi zake kuwa na mabaraza ya Wafanyakazi kwani yanaanzishwa kisheria kwa madhumuni ya kuishauri Serikali katika ngazi za idara, taasisi na Wizara kuhusu usimamizi wa kazi na rasilimali watu, utekelezaji wa majukumu, kulinda haki na wajibu wa waajiri na wafanyakazi, kutoa ushauri kuhusu kujenga hali bora za kazi, maslahi ya Wanyakazi na kusimamia haki na ustawi katika sehemu za kazi. Wajibu wa mabaraza haya kama vyombo vya ushauri na usimamizi ni kuhakikisha kuwa waajiri na watumishi wanatambua wajibu na haki zao, pia wanazingatia maadili ya utumishi wao ili kuleta matokeo ya utendaji wa kazi yenye tija, staha na upendo.

**Ndugu wajumbe**, naambiwa tayari matunda ya kuwa na Baraza la Wafanyakazi mahala pa kazi yameanza kuonekana hapa TIRA. Matunda hayo ni pamoja na kuwashirikisha wafanyakazi katika maamuzi mbalimbali kama vile kuupitia kwa pamoja Mpango Mkakati wa TIRA wa Miaka Mitano (2015/2019), Wafanyakazi kushirikishwa juu ya Mkataba wa Huduma kwa Mteja, na sasa

madhumuni ya mkutano huu ni kuwawezesha wafanyakazi kupitia makadirio ya Bajeti ya Mamlaka kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/2018.

Utaratibu huu unalenga kukuza uwazi na ushirikishwaji katika maamuzi mbalimbali ya Mamlaka ili mfanyakazi anapotekeleza majukumu yake awe akifahamu Mpango Mkakati wa Miaka mitano ijayo wa TIRA unamtaka afanye nini? Vilevile, mfanyakazi wa TIRA anatakiwa kufahamu huduma ya kiwango gani aitoe kwa mteja mara kwa mara. Wakati huo huo, ni lazima ajue bajeti iliyotengwa kwa ajili ya shughuli zake ndani ya Mamlaka ili afanye kazi kwa kuzingatia malengo na rasilimali zilizokadiriwa kutumika.

**Ndugu wajumbe**, Nipende kuwakumbusha kwamba Serikali ya awamu ya tano imedhamiria kwa dhati, kuondoa uzembe na vitendo vyovyote vya rushwa mahala pa kazi hii ikiwa ni pamoja na kubana matumizi yasiyo ya lazima ili kuongeza tija. Hivyo, ni wajibu wa kila mfanyakazi wa TIRA kuhakikisha anafahamu wajibu wake mahali pa kazi, anatekeleza malengo aliyopangiwa katika muda uliopangwa, vile vile anatunza mali na vifaa alivyokabidhiwa kufanyia kazi. Wajibu huo ni pamoja na kuwahi kazini.

**Ndugu wajumbe,** nipende sasa kugusia kidogo kuhusu bajeti itakayowasilishwa kwenu. Naamini TIRA itakuwa imeandaa bajeti yake kwa kufuata utaratibu wa **Medium Term Expenditure Framework (MTEF)**. Utaratibu ambao bajeti huandaliwa kulingana na mipango kazi iliyoainishwa kwenye Mpango Mkakati wa taasisi husika kulingana na vyanzo vya mapato na rasilimali zilizopo.

Mtindo huu wa bajeti huonesha wazi wazi utendaji wa kila idara hususan kwa mtu mmoja mmoja kulingana na vipimo vya utendaji wake. Nichukue nafasi hii kuwataka wafanyakazi wa TIRA kufuata utaratibu unaoelekezwa na bajeti yenu. Tutakapokuwa tunafanya mapitio ya bajeti ya nusu mwaka hapo baadaye, tutaona ni nani au idara gani haikufanya kazi kulingana na malengo ya Mamlaka. Sisi kama Bodi, hatutasita kumwajibisha Meneja yeyote kati yenu ambaye ataonekana kuwa chanzo cha kutotimiza malengo ya Bajeti na Mpango kazi wenu. Hivyo, Ni matumaini yangu kuwa mtaijadili bajeti hii kwa kina ili kila mtu aelewe wajibu gani alio nao ndani ya bajeti hii na jinsi atakavyotekeleza majukumu yake kulingana na utaratibu wa MTEF.

**Ndugu Wajumbe,** Bodi kama chombo chenye kuisimamia Mamlaka na kuhakikisha kuwa utendaji wake uko sambamba na malengo yaliyowekwa na Serikali, itapenda mara kwa mara kujiridhisha na taarifa za robo mwaka kuhusu mapato na matumizi ya fedha, taarifa ya robo kuhusu upanuzi wa soko la Bima hapa nchini, taarifa ya mwaka ya uendelezaji wa rasilimali watu na pia jinsi gani uimara wa soko la Bima unazingatiwa siku kwa siku. Hivyo, ni jukumu la Menejimenti ya TIRA pamoja na Chama cha Wafanyakazi kuhakikisha kuwa wakati wote mnakuwa na mshikamano thabiti ndani ya TIRA ili kuiwezesha Bodi kutimiza majukumu yake ipasavyo. Vinginevyo, kama mtakuwa na migongano kati ya Menejimenti na TUGHE, ufanisi wa kazi hautaonekana na hivyo kuifanya Bodi ishindwe kutimiza azma yake ya kuisimamia vizuri taasisi ya TIRA.

**Ndugu Mwenyekiti na wajumbe,** ningependa kuhitimisha hotuba yangu kwa kusema kwamba ni matumaini yangu mtalitumia baraza hili kuhimiza kila mfanyakazi ajue wajibu wake wa kutumia muda wa kazi ipasavyo kwa kufanya kazi kwa bidii ili kuiwezesha Mamlaka kusonga mbele katika kutekeleza maagizo ya serikali pamoja na huduma kwa wananchi.

Baada ya kusema haya, sasa natamka rasmi kuwa Mkutano wa nne wa Baraza la Wafanyakazi wa TIRA, umefunguliwa rasmi.

**AHSANTENI KWA KUNISIKILIZA.**